



# Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Simu: +255 26 - 2963822  
Nukushi: +255 26 - 296382  
Barua pepe: sg@nbs.go.tz  
Tovuti: www.nbs.go.tz

Barabara ya Jakaya Kikwete  
S. L. P. 2683  
Dodoma  
TANZANIA



Kumb. Na. BE. 424/448/01/57

Tarehe: 09 Februari, 2023

## TAARIFA KWA UMMA KUHUSU WATALII WALIOINGIA NCHINI, UZALISHAJI WA SARUJI NA UMEME, KIPINDI CHA JANUARI - DESEMBA, 2022

Taarifa ya mwenendo wa idadi ya watalii walioingia nchini, uzalishaji wa saruji na umeme ni baadhi ya taarifa za mara kwa mara (high-frequency data) zinazotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa mujibu wa **Sheria ya Takwimu SURA 351**. Viashiria hivi ni baadhi ya vinavyotumika kutathmini mwenendo wa ukuaji wa uchumi wa nchi katika vipindi vifupi.

### **Idadi ya Watalii Walioingia Nchini, Kipindi cha Januari - Desemba 2022**

Idadi ya watalii walioingia nchini katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2022 **iliongezeka hadi 1,454,920** ikilinganishwa na watalii **922,692** walioingia nchini kipindi kama hicho mwaka 2021, ikiwa ni ongezeko la watalii **532,228** sawa na **asilimia 57.7**.

Idadi ya watalii 1,454,920 walioingia nchini mwaka 2022, ilikaribia kufikia idadi kubwa zaidi ya watalii 1,510,151 walioingia nchini mwaka 2019 kabla ya UVIKO-19 **ikiwa ni pungufu ya watalii 55,231 sawa na asilimia 3.7**. Kasi ya ongezeko la watalii nchini baada ya kipindi cha janga la UVIKO-19 inatokana na nchi nyingi kuondoa zuio la wananchi kusafiri nje ya nchi, juhudi za Serikali kutangaza vivutio vya utalii nje ya nchi na kipekee ni kutangaza vivutio vya utalii kupitia filamu ya **“Tanzania, the Royal Tour”** iliyoongozwa na **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan** ambapo matunda yake yameonekana kwa ongezeko la idadi ya watalii kukaribia idadi kubwa zaidi ya watalii walioitembelea Tanzania kabla ya janga la UVIKO-19.

Mwaka 2022, Tanzania ilipokea watalii kutoka nchi mbalimbali ndani na nje ya Bara la Afrika. Watalii walioingia nchini kutoka katika baadhi ya nchi nje ya Bara la Afrika walikuwa kama ifuatavyo: Marekani iliongoza kwa watalii 100,600, ikifuatiwa na Ufaransa (watalii 100,371), Ujerumani (watalii 67,718), Uingereza (watalii 60,116) na Poland (watalii 46,431). Katika Bara la Afrika, watalii wengi walioingia Tanzania walitoka katika nchi za: Kenya (watalii 166,324), Burundi (watalii 100,851), Zambia (watalii 46,787), Malawi (watalii 44,438) na Rwanda (watalii 44,288). Aidha, nchi 10 kati ya 214 ziliingiza watalii wengi zaidi waliofikia **watalii 778,918** ikiwa ni sawa na **asilimia 53.5** ya watalii wote.

### **Uzalishaji na Matumizi ya Saruji Nchini, Kipindi cha Januari - Desemba 2022**

Matumizi ya saruji katika nchi yanatumika kama kiashiria cha kutathmini ukuaji wa shughuli za kiuchumi hususan za ujenzi wa miundombinu na nyumba kwa ajili ya matumizi mbalimbali kama vile makazi na biashara.

Matumizi ya saruji nchini mwaka 2022 yaliongezeka hadi tani 7,823,361 kutoka tani 6,863,004 mwaka 2021 ikiwa ni ongezeko la **tani 960,356** sawa na **asilimia 14.0**. Mwenendo huu

unaakisi kuendelea kuongezeka kwa ujenzi wa miundombinu na ujenzi wa nyumba hapa nchini.

Katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2022, saruji iliyozalishwa nchini iliongezeka hadi tani 7,598,073 kutoka tani 6,614,359 kipindi kama hicho mwaka 2021 ikiwa ni ongezeko **tani 983,714 sawa na asilimia 14.9**.

Takwimu za biashara nje ya nchi zinaonesha kuwa, mwaka 2022 kiasi cha saruji kilichouzwa nje kiliongezeka hadi tani 491,538 kutoka tani 441,828 mwaka 2021 ikiwa ni ongezeko la **tani 49,710 sawa na asilimia 11.3**. Aidha, kiasi cha saruji kilichoingizwa kutoka nje ya nchi katika kipindi hicho kiliongezeka hadi tani 716,826 kutoka tani 690,474 mwaka 2021 ikiwa ni ongezeko la **tani 26,356 sawa na asilimia 3.8**.

### **Uzalishaji na Matumizi ya Umeme Nchini, Kipindi cha Januari – Desemba 2022**

Mwaka 2022, matumizi ya umeme yaliendelea kuongezeka hadi saa za kilowati milioni 9,462.3 kutoka saa za kilowati milioni 7,994.8 mwaka 2021, ikiwa ni ongezeko la saa za kilowati **milioni 1,467.4 sawa na asilimia 18.3**.

Uzalishaji wa umeme uliongezeka hadi saa za kilowati milioni 9,312.0 mwaka 2022 kutoka saa za kilowati milioni 7,850.8 mwaka 2021 ikiwa ni ongezeko la saa za kilowati **milioni 1,461.2 sawa na asilimia 18.6**. Aidha, uzalishaji wa umeme kwa kutumia chanzo cha gesi asilia uliongezeka hadi saa za kilowati milioni 6,635.9 mwaka 2022 sawa na **asilimia 71.3** ya umeme wote uliozalishwa. Vilevile, saa za kilowati milioni 5,033.9 zilizalishwa kwa kutumia gesi asilia mwaka 2021 sawa na **asilimia 64.1** ya umeme wote uliozalishwa.

*Kwa taarifa zaidi wasiliana na Mtakwimu Mkuu wa Serikali S.L.P 2683 Dodoma, Simu +255 26 2963822, Nukushi +255 26 296382, Barua pepe: [sg@nbs.go.tz](mailto:sg@nbs.go.tz), tovuti: [www.nbs.go.tz](http://www.nbs.go.tz)*

